# Reli ya SGR yaifungua Tanzania kimataifa

## >>> **Rais** wa Burundi, Ndayishimiye, Waziri Mkuu Majaliwa waweka jiwe la msingi ujenzi wa SGR kutoka Uvinza hadi Musongati nchini Burundi

## >>> **Ujenzi** wake kugharimu dola za marekani bilioni 2.154, ujenzi wa reli hiyo, wataja kukuza ushirikiano wa kibiashara na kiuchumi



WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa akisalimiana na Rais wa Jamhuri ya Burundi Meja Jenerali Evariste Ndayishimiye wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR)

Ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR imekuwa ndio dira ya Serikali ya Awamu ya Sita ambapo imesimama imara katika kujenga reli hiyo ambayo sasa inatoa huduma bora na kwa ufanisi mkubwa kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma.

**NA MWANDISHI WETU, BURUNDI**

SEKTA ya uchukuzi imekuwa na mafanikio makubwa katika Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha miradi ya kimkakati inajengwa.

Lengo la kufanya hivyo ni kukuza uchumi kupitia sekta ya usafiri na usafirishaji ikiwa ni maelekeo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025 ambaye serikali imetekeleza kwa ufanisi ikiwemo kuendeleza na kujenga miradi mingi.

Ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR imekuwa ndio dira ya Serikali ya Awamu ya Sita ambapo imesimama imara katika kujenga reli hiyo ambayo sasa inatoa huduma bora na kwa ufanisi mkubwa kuanzia Dar es Salaam hadi Dodoma.

Haya ni matunda makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita ambapo sasa nguvu hiyo imeelekezwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambapo ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Uvinza (Tanzania) na Msongati (Burundi) umeanza.

Ujenzi huo umetajwa kukuza ushirikiano wa kiuchumi katika nyanja mbalimbali ikiwemo sekta ya usafiri na usafirishaji ambapo unakwenda kuandika historia kubwa kwa mataifa hayo mawili kupitia usafiri huo.

Hatua hiyo inatokana na malengo ya viongozi hao wa Burundi na Tanzania kunuia kufungua nchi hizo kupitia ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR kutoka eneo la Uvinza (Kigoma) nchini Tanzania hadi Musongati nchini Burundi.

Ujenzi wa reli hiyo ya kisasa umetajwa kuwa na faida lukuki kwa wananchi wa maeneo hayo mawili ambayo yanasifika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi ambapo kupitia ujenzi wa reli hiyo uchumi wa wananchi hao utakuwa maradufu.

WAZIRI MKUU MAJALIWA

Akizungumza katika uwekaji wa jiwe la msingi wa reli hiyo Agosti 16, 2025, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema uwekaji wa jiwe la msingi ni safari ya maendeleo kwa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kupitia reli ya kisasa ya SGR.

"Leo (Jumamosi, Agosti 16, 2025) tumeshiriki uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa reli ya kisasa ya kutoka Uvinza hadi Musongati na kuwahahikishia Watanzania na WanaBurundi kwamba ujenzi huo utaanza katika muda uliopangwa." Alisema

Aliongeza; "Viongozi wetu kwa upande wa Tanzania, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na nchini Burundi, Evariste Ndayishimiye wamekuwa na dhamira njema kuhakikisha ujenzi wa reli hiyo unakamilika kwa wakati na kuwa na mafanikio."

Waziri Mkuu ambaye ameshiriki hafla hiyo kwa niaba ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema reli hiyo itakayokuwa na urefu wa km.240 pindi ikikamilika, itakuwa ndiyo reli ya kwanza inayounganisha nchi na nchi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

"Hii ni reli ya mfano na itaandika historia kubwa kutokana na kuweza kuunganisha nchi moja kwenda nyingine. Kila mwananchi anapaswa kujivunia dira na maono makubwa ya viongozi wetu wa Burundi na Tanzania kwenda kujenga reli hii." alisema

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika eneo la Musongati, Burundi, Waziri Mkuu Majaliwa, alisema kukamilika kwa ujenzi wa reli hiyo kutasaidia kuunganisha masoko na kuendeleza biashara baina ya Tanzania na Burundi.

Alieleza; "Reli ikikamilika itafungua fursa kwa wananchi wetu ambao wataweza kutoka hapa hadi Dar es Salaam ndani ya siku moja. Hata kwenye usafirishaji wa mizigo, hivi sasa, lori linatumia saa 96 kutoka Dar hadi Bujumbura lakini baada ya kukamilisha ujenzi, usafirishaji wa mizigo kwa kutumia treni utatumia saa 20 tu."

"Mradi wa reli ya kisasa siyo tu kwamba utarahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo, bali pia utafungua milango ya fursa mpya za uwekezaji na biashara kati ya Tanzania na Burundi. Kutokana na maeneo hayo kuwa na fursa kubwa kibiashara" alisema

Akielezea kuhusu mradi huo, Waziri Mkuu amesema ujenzi wa reli hiyo utagharimu dola za Marekani bilioni 2.154 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miaka mitano na kwamba mwaka mmoja baada ya ujenzi utakuwa ni wa matazamio.

**RAIS WA BURUNDI**

Kwa upande wake, Rais wa Burundi, Meja Jenerali Evarist Ndayishimiye alisema kuanza kwa ujenzi wa reli hiyo kutatibu shauku ya muda mrefu ya nchi hiyo kuwa na usafiri wa reli ambao unakwenda kukuza uchumi wa taifa hilo.

"Leo ni siku ya furaha sana kwetu. Tumepata jawabu la tangu enzi na enzi. Mwaka 1921, mradi huu ulianzishwa na Wabelgiji kisha wakaja Wajerumani lakini wakashindwa. Leo hii Tanzania na Burundi tumeweza," alisema.

Alisema Burundi imebarikiwa kuwa madini mengi na kuna wakati aliitisha kikao cha wawekezaji kutoka nchi kadhaa, lakini usafiri na usafirishaji imekuwa changamoto kubwa, hivyo ujenzi wa reli hiyo ni jawabu la matatizo ya nchi hiyo kukua kiuchumi.

"Niliwahi kuwaita wawekezaji na wengi walivutiwa na wakataka kuwekeza mara moja, lakini wakaniuliza, tukianza kuchimba madini ya Nickel, tutayasafirishaje?. Ujio wa reli hii ni moja ya hatua madhubuti ya kuwakwamua kiuchumi wananchi wa Burundi" alisema

Alieleza; "Changamoto ya ukosefu wa usafiri wa reli ulitufanya tubungue bongo zetu na kutafuta suluhisho. Tunaishukuru sana Serikali ya Tanzania kwa kukubali kuungana nasi ili tuanze mradi huu muhimu."

Rais Ndayishimiye alisema "Tukitoka hapa, tunataka reli iunganishe hadi Kindu, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC). Na baada ya hapo, tunataka reli yetu ifike Afrika Magharibi kwenye ufukwe wa bahari ya Atlantiki kwani tunaamini njia hiyo itaharakisha kuleta maendeleo."

Rais Ndayishimiye alimpongeza Rais Dkt. Samia kwa kufikia hatua kubwa za maendeleo ikiwemo kuweka msukumo mkubwa ujenzi wa reli hiyo ambayo inakwenda kufungua milango ya kiuchumi kwa wananchi wan chi hizo mbili.

"Ukirudi nyumbani mwambie Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan kwamba tunampongeza sana kwa kuleta maendeleo ya haraka nchini Tanzania." Alisema rais Ndayishimiye na kuamsha shangwe kubwa kwa wananchi waliohudhuria hafla hiyo.

"Nimekaa Tanzania kwa muda mrefu lakini kwa sasa nikija naweza kupotea. Magomeni napajua, Tabata na Vingunguti napajua, Mwenge napajua, na Kinondoni nilishakaa; lakini kwa sababu ya maendeleo yaliyopatikana, naweza kupotea." Alisema




WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa na Rais wa Jamhuri ya Burundi Meja Jenerali Evariste Ndayishimiye.



WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa na Rais wa Jamhuri ya Burundi Meja Jenerali Evariste Ndayishimiye wakisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) Mhandisi Machibya Masanja.

Aliongeza; "Tunamshukuru kwa uongozi wake imara, Amekuwa kiongozi oimara na mwenye maono makubwa katika kuleta maendeleo kwa Watanzania na anamtakia kheri kubwa katika uongozi wake"

Katika hafla hiyo, Rais Ndayishimiye alikonga nyoyo za watu wengi kutokana na kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasahi na uweledi mkubwa na kuamsha shangwe kubwa miongoni mwa wananchi waliohudhuria tukio hilo.

**WAZIRI MBARAWA**

Awali, Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alisema utekelezaji wa mradi huo unaenda sambamba na Ajenda 63 ya Umoja wa Afrika ambayo inataka bara la Afrika liunganishwe kwa mtandao wa reli ya kisasa.

Alisema mbali na kuziunganisha nchi hizo mbili, kukamilika kwa ujenzi wa reli hiyo, kutarahisisha kupunguza gharama za usafirishaji wa mizigo ambapo sasa inatumika gharama kubwa kusafirisha mizigo kutoka Tanzania hadi Burundi.

Alieleza; "Hivi sasa, kontena moja la futi 20 linasafirishwa kwa gharama ya dola za Marekani 3,800 lakini reli ikikamilika, gharama itashuka hadi dola za Marekani 2,000. Haya ni mageuzi makubwa kwa sekta ya usafirishaji"

Alisema faida nyingine itakayopatikana baada ya mradi huo kukamilika ni kuwezesha kusafirisha mizigo mingi kwa wakati mmoja na kuondoa muda wa kusafirisha mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Hivi sasa, mzigo unaosafirishwa kwa lori moja ni tani 30, lakini reli ikianza kazi, tutaweza kusafirisha tani 3,000 kwa wakati mmoja. Haya ni mageuzi makubwa na mzigo unaweza kusafirishwa kwa siku moja," alisema Waziri Mbarawa.

HISTORIA YA UJENZI WA RELI YA SGR UVINZA HADI MUSONGATI

Tanzania imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha mfumo bora wa usafirishaji unaboresha ikiwemo kukuza uchumi wake kupitia njia kuu za usafiri na usafirishaji ikiwemo reli, anga, barabara na maji ambapo kwa reli imekuwa ikijenga vipande mbalimbali vya sgr.

Tanzanai tayari imekamilisha ujenzi wa SGR kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma huku ikiendelea na ujenzi wa maeneo mengine ikiwemo kutoka Makutopora- Tabora hadi Kigoma na kipande cha Makutupora hadi Mwanza.

Lengo la ujenzi wa reli ya SGR na kuhakikisha uchumi wan chi unakuwa na wananchi wanaweza kufanya shughuli zao za kiuchumi kutoka eneo moja hadi nyingine ambapo kukamilika kwa ujenzi wa kipande cha Uvinza hadi Musongati kinakwenda kubadirisha uchumi wa mataifa hayo mawili.

Januari 22, 2022 Tanzania na Burundi iliingia makubalia ya ujenzi wa reli hiyo yenye urefu wa kilomita 282 ikiwa ni mwendelezo wa ujenzi wa kipande cha reli ya kisasa kutoka Tabora hadi Uvinza. Ujenzi wa reli hiyo unakwenda kuibua fursa nyingi za ajira kwa wananchi.

Mwananchi Ijumaa Agosti 22, 2025, pg9




Abiria wakisaidia kusukuma daladala iliyoharibika katikati ya Barabara ya Mandela eneo la Tabata Relini jijini Dar es Salaam jana na kusababisha foleni kwa magari. **Picha na Said Khamis**

CS CamScanner